(١)

ترجمة الخطبة إلى اللغة السواحيلية

Ujenzi wa Uchumi Bora na athari
yake kwa Utulivu wa Jamii.

Sifa zote ni zake Mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa viumbe vyote, ambaye anasema katika Kitabu chake Kitukufu:
Hakika yeye amekuumbeni kutokana na ardhi na akakujaalieni kuijaza ardhi hiyo. Na ninashuhudia kuwa hakuna mungu mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, ni yeye pekee asiye na mshirika wake, na ninashuhudia kuwa Bwana wetu Muhammad S.A.W ni Mja na Mjumbe wake. Na baada ya Utangulizi huu.

Hakika Uchumi wenye nguvu ni miongoni mwa nguzo imara za nchi na ni tegemeo lake la kimsingi ambalo nchi haiwezi kusimama au kujengwa isipokuwa kwayo. Kwani uchumi tulivu wenye nguvu huiwezesha nchi kutekeleza majukumu yake ya ndani na ya nje na kuwawekea wananchi wake maisha bora. Na uchumi unapozorota, ufukara na magonjwa huenea na maisha huyumba na mgogoro huzuka pamoja na maadili kuharibika na kuongezeka uhalifu na huwa fursa kubwa kwa maadui wanaozinyemelea nchi hizo ambao wanafanya juhudi za kuziangusha na kuziingiza katika wimbi la machafuko lisilokwisha

Kwa hivyo Mtume Muhammad S.A.W alikuwa akijikinga na Ufakiri baada ya kila swala kwa kusema: Ewe Mola wangu, mimi ninajikinga kwako na Ukafiri, na Ufukara na adhabu ya Kaburini.
Hakika Taifa lisilomiliki au kuzalisha nguvu zake, Chakula chake, Nguo zake, Dawa zake, Silaha zake, halina uwezo wa kumiliki mambo yake, Utashi wake, Neno lake, Utukufu wake na Heshima yake. Na hakika wamesema wenye Hekima: Msaidie umtakaye utakuwa na amri juu

yake, na epukana na umtakae utakuwa mpinzani wake, na uhitaji kitu kwa mtu utakuwa mateka wake

Na Dini yetu Tukufu ya Uislamu, imetufundisha kuwa Mkono uliyo juu ni bora kuliko Mkono ulio chini, ambapo Mtume wetu Muhammad S.A.W anasema: (Mkono uliyo juu ni bora kuliko Mkono ulio chini). Na anasema Mtume Muhammad S.A.W: (Mkono unaotoa ndiyo ulio juu na Mkono unaoomba ndiyo ulio Chini). Na hakuna Shaka yoyote kuwa haya yanahusu Mataifa na Taasisi mbali mbali pamoja na familia na pia mtu mmoja mmoja. Hakuna Taifa lolote, taasisi yoyote au hata familia yoyote inazoweza kuendelea isipokuwa kwa kuwepo sababu maalumu ambazo ni: Kufanya kazi na kuongeza uzalishaji. Na kinachotakiwa sio kuongeza uzalisha tu bali kuongeza uzalisha pamoja na ufanisi, ubunifu, uvumbuzi na kuingia katika Nyanja zlizo hai zaidi na zenye pato kubwa zaidi la kiuchumi. Kwani kazi na Uzalishaji ni takwa la kisheria na ni wajibu wa kitaifa. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuamrisha kuhangaike ardhini baada ya kutekeleza Haki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambapo anasema: {Na pindi Swala itakapomalizika basi sambaeni ardhini na mzitafute fadhila za Mwenyezi Mungu na mumtaje kwa wingi Mwenyezi Mungu huwenda nyinyi mkarehememewa}. Na kwa hiyo, Dunia inajengwa kwa kufanya kazi, na ukhalifa wa Mwanadamu unapatikana ndani ya Dunia hii kwa kazi, na kwa kufanya kazi mtu anaulinda utu na heshima yake. Kwani mtu mwenye sifa hizi huwa anawapa watu na wala hawaombi, na hutoa bila ya kuuliza. Na Mtume Rehma na Amani zimfikie ametuambia kuwa chakula kilicho bora ambacho mtu anakila ni kile alichokichuma kwa tabu na juhudi zake mwenyewe, ambapo anasema: Mtu yoyote hali chakula kilicho bora zaidi kamwe kuliko kula chakula kilichopatikana kwa jasho lake. Na kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu DAudi rehma na amani zimfikie, alikuwa anakula chakula kilichotokana na kazi za mikono yake. Na hakika Mtume Rehma na amani zimfikie ametoa onyo kali kwa Mtu

yoyote atakaeupenda Uzembe na starehe, na akajipatia chakula chake kwa kuwaomba watu. Akasema Mtume: (Mmoja wenu ataendelea kuomba omba mpaka akakutana na Mola wake Mtukufu huku akiwa hana hata kipande kidogo cha nyama za uso wake). Na Bwana wetu Omar radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie, alikuwa anasema: Jiepusheni na starehe, hakika hiyo ni kujisahau.

Uislamu umeipa kazi thamani ya juu, na ukaifanya kazi kuwa katika daraja za juu za Ibada, nayo ni jihadi katika njia ya mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwani mja analipwa kwa ibada hii ya kazi. Na ikiwa mtu ataiaga Dunia akiwa kazini basi kifo chake kitakuwa katika hali ya Utiifu wa Mola wake. Kutoka kwa Kaab bin Ujrah Radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie amesema: Mtu Mmoja alipitia kwa Mtume Rehma na Amani zimfikie, na Maswahaba wa Mtume rehma na amani zimfikie wakaona juhudi na uchangamfu wake, kisha wakasema: Ewe Mtume wa MWenyezi Mungu, Je kama juhudi hii na uchangamfu huu ungelikuwa katika njia ya Mwenyezi Mungu ingekuwaje? Mtume rehma na amani zimfikie akasema: (Ikiwa Mtu huyu ametoka kwa ajili ya kumuhangaikia watoto wake wadogo basi yeye yuko katika njia ya Mwenyezi Mungu, na ikiwa ametoka kwa ajili ya kuwahangaikia wazazi wake waliozeeka basi yeye yuko katika njia ya Mwenyezi Mungu, na ikiwa yeye anajihangaikia mwenyewe kwa ajili ya kuikinga nafsi yake isiombe vya watu basi yuko katika njia ya Mwenyezi Mungu, na ikiwa atakuwa ametoka kwa ajili ya kuwaonesha watu tu na kujivuna basi atakuwa katika njia ya Shetani. Na katika wito wa uzalishaji .

Kimetafsiriwa na
profesa\ Ayman Alasar